

Jina.....

Nambari yako.....

Shule.....

Sahihi yako.....

Tarehe.....

102/3

KISWAHILI

FASIHI

KARATASI YA 3

Julai/Agosti 2012

Saa 2 ½

**JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA ZA MBITA – SUBA – 2012**  
*Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E.)*

102/3

KISWAHILI

FASIHI

KARATASI YA 3

Julai/Agosti 2012

Saa 2 ½

**MAAGIZO**

- (a) Jibu maswali **manne** pekee
- (b) Swali la **kwanza** ni la **lazima**.
- (c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani:  
Tamthilia, Hadithi Fupi, Fasihi simulizi na Riwaya
- (d) Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja.
- (e) Andika kila jibu kwenye ukurasa mpya.

*Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa*

*Watahiniwa wanastahiliku hakikisha kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa*

**A: USHAIRI**

**1. Lazima**

**Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Kimya changu kimezidi, navunja yangu subira,  
Merejeya kwa miradi, kuhitimisha dhamira,  
Kukejeli sina budi, niwafunze utu bora,  
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Sirikali bila hadi, ndo kiini cha madhara,  
Yanopiga kama radi, isokuwa na ishara,  
Yamini kuwa gaidi, wakitupora mishahara,  
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Wamejifanya hasidi, wasopatana kifikra,  
Wana yao maksuudi, kujizombea ujira,  
Wakilenga kufaidi, tumbo zao za kichura,  
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Nchi yetu kufisidi, ni jambo linonikera,  
Tangia siku za jadi, ufukara ndo king'ora,  
Kutujazeni ahadi, nyie mkitia fora,  
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Maskini watozwa kodi, wapwani na walo bara,  
Kwa uvumba na uudi, mwawalipa kwa hasara,  
Hamudhamini miradi, mejihisi masogora,  
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Mesema kazi ni chudi, basi sirikali gura,  
Nafsi zenu mzirudi, mkubali kuchakura,  
Makondeni mkirudi, muondoe ufukara,  
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Ujanjenu umezidi, demokrasia bakora,  
Debeni takaporudi, michirizi kwenye sura,  
Kuwachuja a! muradi, kwa za mkizi hasira,  
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

## Maswali

1. (a) Toa anwani mwafaka kwa shairi hili (alm1)
- (b) Ainisha shairi hili kwa jinsi tatu na kutoa sababu. (alm3)
- (c) Onyesha mbinu za lugha katika shairi hili. (alm2)
- (d) Bainisha matumizi matatu ya uhuru wa mshairi katika shairi hili. (alm3)
- (e) Andika ubeti wa nne katika mtindo tutumbi. (alm4)
- (f) Fafanua maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. (alm3)
- (g) Taja mpango mmoja unaotajwa kama njia ya kutatua matatizo ya nchi. (alm1)
- (h) Eleza muundo wa shairi hili. (alm3)

## B: TAMTHILIA

### Kifo Kisimani: Kithaka wa Mberia.

2. “Msijali utawala wa Mtukufu Mtemi Bokono utahakikisha uovu huo umekomesha Kabisa...”
  - (a) Liweke dondoo hili katika muktadha wake. (alm4)
  - (b) Ni uovu gani unaorejelewa katika dondoo hili. (alm2)
  - (c) Ukirejelea tamthilia ya Kifo Kisimani onyesha kwa kutoa mifano, visa vingine sita vya uovu katika Butangi. (alm12)
  - (d) Msemaji wa kifungu hiki alikuwa chui aliyevalia ngozi ya kondoo. Thibitisha (alm2)
3. Onyesha vile wanawake walivyosifiwa katika Kifo Kisimani. (alm20)

## C: HADITHI FUPI

### Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi zingine.

4. Watoto katika jamii wanakabiliwa na matatizo chungu nzima. Jadili ukirejelea diwani ya Mayai Waziri wa Maradhi. (alm20)
5. Kachukua hatua nyingine.  
“Shida na dhiki iliendelea kuwaninginia juu kama mikanda ya masizi iliyokuwa kwenye jiko lao dogo....”
  - (a) Liweke dondoo hili katika muktadha wake. (alm4)
  - (b) Tambua kwa kutoa mfano, tamathali ya usemi iliyotumiwa katika dondoo. (alm2)
  - (c) Tambua shida na dhiki sita zilizowazonga warejelewa wa dondoo. (alm6)
  - (d) Ugumu wa maisha unaowakumba wasemewa kwenye dondoo ni msiba usiokuwa na kilio. Tetea. (alm8)

**D: FASIHI SIMULIZI**

6. (a) Fafanua sifa tatu za :- (alm9)
- (i) Tendi
  - (ii) Soga
  - (iii) Lakabu
- (b) Eleza umuhimu wa nyimbo katika usimulizi wa hadithi. (alm5)
- (c) Taja na kueleza vipera vyovyote vitatu vya hadithi. (alm6)

**E: RIWAYA**

**Utengano: S.A. Mohamed**

7. Hadithi ndani ya hadithi ni mbinu aliyoitumia barabara mwandishi. Fafanua. (alm20)
8. Moyo ulimkutuka, lakini alijiasa kutulia. Alingojea tena kwa kitambo. Hatimaye akaamua Kutoa kikohozi. Kikohozi cha Maksuudi...
- (a) Unafikiri ni kwa nini mhusika huyu alijiasa kutulia? (alm4)
  - (b) Eleza umuhimu wa mhusika anayerejelewa hapa. (alm6)
  - (c) Jadili maudhui yoyote mawili yanayojitokeza kutoka kwenye muktadha huu. (alm6)
  - (d) Eleza hatima ya kungojea huku kwa mhusika huyu. (alm4)